KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na By Eric Louw

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

JUMA LA PILI: APRILI 03 – APRILI 09, 2020

VIPI TUKITAZAMA DHAMBI KAMA TUNAVYOITAZAMA COVID-19?

Majuma kadhaa yaliyopita, mimi na mke wangu wote tulipatwa na homa tuliyodhani kwamba imetokana na chakula chenye sumu. Tunashukuru, baada ya saa 36 za kupambana na homa, mimi nilipona. Hata hivyo, homa ya mke wangu, haikutoka. Aliendelea kuwa na kikohozi kikavu na maumivu ya mwili.

Baada ya siku chache, tuliwapigia simu wahusika wa kitengo kinachopima COVID-19 na kupanga nao muda wa kwenda kuwaona ili kupima. Baada ya kuwaeleza kuhusu zile dalili, tualiambiwa kwamba, ingawa alikuwa na dalili zote zinazofanana, vinginevyo kama anajua kwamba alikutana na mtu aliyepimwa na kukutwa na COVID -19, hangetakiwa kupimwa tena. Kwenda kupima tena ingekuwa ni kupoteza muda.

Siku chache baadaye, huku akiendelea kupambana na homa, mke wangu aliamka akiwa anakohoa makohozi mazito. Jambo lile lilimstua sana kiasi kwamba alianza kukohoa na kutapika na hakuweza kutulia kwa takriban saa mbili. Tulimpeleka kwenye chumba cha dharura tukamweleza daktari hayo yote hapo juu. Walimpa huduma ya dawa kupitia mishipa yake ya damu, ambayo ilimsaidia na kudhibiti mambo.

Niliwauliza tena juu ya uwezekano wa mke wangu kupimwa COVID-19, ikizingatiwa kwamba huwa anafanya kazi na watu wengi wa kimataifa na pia hivi karibuni tulikuwa tumehudhuria kongamano kubwa nje ya jimbo letu. Madaktari walisema kwamba, hata kama mke wangu alikuwa na dalili, kupimwa kulihitaji awe amekutana na mtu aliyepimwa na kuonekana kuwa ana COVID-19.

Madaktari walipokuwa wanatuambia jambo hilo, niligundua kuwa labda kulikuwa na upungufu wa vifaa vya kupimia, au wataalamu wa afya walikuwa wanasubiri ugonjwa uenee kwenye jamii, ndipo waanze kuchukua vipimo kwa umkini.

Baada ya majadiliano zaidi, hatimaye daktari alitwambia kwamba mke wangu angefanyiwa vipimo vya kila kitu. Kama majibu yangekuwa hasi, zile sampuli zingepelekwa haraka kwenye idara mahalia ya afya kwa ajili ya kupima COVID-19, na tungerudi pale ndani ya siku kadhaa. Kwa wakati huo tulielekezwa kurudi nyumbani na kujiweka kwenye karantini, jambo hilo tulilifanya.

Wakati vipimo vya mwanzo kwa ajili ya kila kitu viliporudi na kuonesha HASI, ile siku ya kwanza nililijulisha kila kundi la watu nililokutana nalo juu ya hali yetu ili kuzidisha tahadhari.

Bila kuhitaji kuwashumbua sana wengine, niliamua kuwasiliana na hospitali ili kujua iwapo sampuli ya mke wangu ilikuwa imepelekwa kwa ajili ya kipimo cha COVID-19. Wafanyakazi wa pale hawakujua sampuli ile ilikopelekwa. Nilipiga simu sehemu moja hadi nyingine na sikupata taarifa za kunisaidia. Ilichukua muda mrefu, hatimaye ndipo nilipounganishwa na Mtaalamu wa Wilaya wa magonjwa ya mripuko na kugundua kuwa hawakuwa na mpango wa kupeleka sampuli kwa ajili ya kupima. Nilipomwelezea juu ya hali iliyopo na namna watu walivyowekwa kwenye karantini wakisubiri matokeo, alisema wangepima sampuli COVID-19 siku ya Jumanne.

Siku ya Jumanne ilifika ikaondoka. Hakuna majibu. Jumatano ilifika ikaenda. Hakuna majibu. Wakati huo mke wangu aliishia kurudishwa kwenye chumba cha dharura, maana aliendelea kukohoa, hakuweza kujizuia. Alhamisi ilifika nayo ilikuwa inaendelea kwenda. Hakuna majibu. Baada ya kuulizia tuligundua kuwa kulikuwa na mrundikano wa sampuli zimesubirishwa, huenda zikiwa na visa vilivyofanana na chetu. Hatimaye, Alhamisi saa 1:30 usiku, karibu siku 12 tangu karantini ya kwanza, ndipo matokeo yalipokuja. NEGATIVE! Tulipata wepesi sana, lakini ufumbufu ulikuwa mkubwa!

Huo uzoefu wetu, unanikumbusha kwa njia nyingi juu ya “Kirusi” cha kwanza. Kama ilivyo COVID-19 dhambi, ilipogunduliwa kwanza pale mbinguni, haikuonekana kuwa ni ya kufisha. Hata ilipowasili hapa duniani haikuonekana kama ni ya kufisha ki vile, maana ilikuwa imejiweka “karantini” kwenye mti mmoja tu. Lakini dhambi ilipoanza kusambaa kutoka kwa Nyoka hadi kwa Hawa na kisha kwa Adamu na wazao wao, ilikua haraka na kuwa kitu ambacho hakiwezi kudhibitiwa kabisa.

Kwa bahati mbaya, kinyume na mwitikio wa ulimwengu dhidi ya COVID-19, wengi wetu hatujali kuhusu kusambaa kwa dhambi. Hatuna wasi wasi kuhusu kuyapima maisha yetu kwa Neno la Mungu na kuichunguza mioyo yetu. Lakini tunapuuzia hizo dalili – ubinafsi, hasira, kiburi – vinajidhihirisha katika kila jambo tunalofanya. Tunafurahia dhambi, tunacheza nayo, tunataniana juu ya dhambi, lakini hatujaribu kuisafisha katika maisha yetu kwa gharama zote.

Vipi kama tungefanya mambo tofauti? Vipi kama dhambi tungeitendea kama tunavyoitendea COVID-19?

Zaburi 139: 23, 24

“Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, Unijaribu, uyajue mawazo yangu; 24 Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, Ukaniongoze katika njia ya milele.” Mungu anatamani sana tuweze kujijua hali yetu ya kweli na kutafuta uponyaji wa kiroho. Moyo wake unatamani sisi tupate kusafishwa na kutakaswa. Sote tupo kwenye karantini hapa duniani, lakini siku moja hivi karibuni hii karantini itafika mwisho na Yesu atakuja kutuchukua na kutupeleka nyumbani. Atakapo kuja, wewe utakuwa tayari?

Eric Louw ni mchungaji katika Konferensi ya Texas, kwa sasa ni mwanafunzi wa shahada ya Uzamivu (MDiv), Andrews University

Maswali ya Moyoni

Je! Tunatamani kumpa Mungu ruhusa ya kuichunguza mioyo yetu na kutusafisha kutokana na kirusi cha kufisha cha dhambi? Vipi ikiwa kufanya hivyo ni kuomba msamaha kutoka kwa mtu fulani ambaye dhambi zetu zimemjeruhi?

Changamoti Hai ya Moyoni

Juma hili, kadiri tunavyoendelea kuomba kwa ajili ya ulinzi wa kiroho na uponyaji, hebu tuombe kwa dhati kwa ajili ya uponyaji wetu wa kiroho. Na hebu tuchukue hatua na kuwafikiwa watu wanaotuzunguka- kuomba msamaha, kutafuta upatanisho, na kushiriki na wengine upendo wa Mungu! Hebu tusiifanye dhambi kuwa ni ndogo au kubwa tena, lakini tuombe Mungu atusaidie kuikimbia kwa nguvu zetu zote. Tunapoomba, hebu tudai ahadi iliyoandikwa katika 1 Yohana 1:9 na Isaya 1:18.

“Wengi ambao wangesinyaa kwa kitisho cha makosa makubwa wanaongozwa kuona kuwa dhambi katika mambo madogo kuwa ina matokeo rahisi. Lakini hizi dhambi ndogo zinadhoofisha maisha ya utauwa ndani ya roho.” (The Faith I live By, uk. 92)

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili

- Ellen White, *Steps to Christ,* chapters 2-3
- *“Removing the Spiritual Breaches”*
  Tembelea: www.revivalandreformation.org

SIKU YA 8 - MAMBO YA KUOMBEA

Ijumaa, Aprili 03, 2020

1. Kuombea nchi na maeneo ambayo yameathirika sana na janga la COVID-19, zenye vifo vingi na mifumo ya afya iliyozidiwa.

2. Kuomba kwa ajili ya uvumilivu na uwezo wa wataalamu wa afya. Kama unamfahamu mtaalamu ye yote wa afya, hebu mfanye ajue kuwa unamwombea.

3. Omba neema ya Mungu kwa ajili ya washiriki wa kanisa mahalia wanaokabiliana na mabadiliko mengi yanayotokea katika maisha ya kila siku. Waombee ambao tayari wameathirika ili kwamba waweze kuchukuliana na hali, na zaidi ya hapo wawe mashahidi waaminifu kwa uongozi wa Mungu wenye nguvu katika maisha yao.

4. Omba kwamba washiriki watafute njia bora za kutiana moyo katika imani, na kwa namna ya pekee wawatie moyo wale wanaopitia uzoefu wa karantini na kutengwa peke yao.

5. Tuwaombee watu walioko kule Mindanao North Eastern Mission, Ufilipino wanaopambana na ukosefu wa chakula na mahitaji mengine muhimu wakati huu wa janga la COVID-19. Tuombe kwamba imani zao ziimarike.

SIKU YA 9 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumamosi, Aprili 04, 2020

“Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. (Warumi 8:13)”

AA, 9
“Kanisa ni uwakala wa Mungu ulioteuliwa kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Liliundwa kwa ajili ya huduma, na utume wake ni kupeleka injili ulimwenguni. Tangu mwanzo ulikuwa ni mpango wa Mungu kwamba kwa njia ya kanisa lake uaminifu wake na utoshelevu wake uweze kuakisiwa kwa ulimwengu. Washiriki wa kanisa, ambao aliwaita kutoka gizani hadi kwenye nuru ya ajabu, wanatakiwa kuonesha utukufu wake. Kanisa ni hazina ya utajiri wa neema ya Kristo; na kwa njia ya kanisa, hatimaye onesho kamili la mwisho la upendo wa Mungu litadhihirika, hata kwa “falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho”

1. Tuombe kwamba sisi Waadventista wa Sabato tuweze kukamilisha utume wetu kama mawakala tulioteuliwa na Mungu kwa ajili ya wokovu wa wanadamu.

2. Tuwaombee baadhi ya washiriki wetu kule Kenya. Tuombee msamaha na uponyaji miongoni mwa washiriki wa kanisa, na umoja na hekima ya namna ya kuenenda katikati ya janga la COVID-19. Omba kwamba Roho Mtakatifu awe pamoja na viongozi wa kanisa katika nchi yote ya Kenya.

3. Tuombe kwa ajili ya washiriki na viongozi wa kanisa wanaoendelea kunyanyaswa kule Burundi. Tuombe ili kwamba upendo wa Mungu uonekane kupitia ushuhuda wa wale walioko Burundi na kupitia ushuhuda wa washiriki wa kanisa ulimwenguni kote, wanaoangaza kwa ajili ya Yesu hata katikati ya tufani na mateso.

4. Tuombee msisitizo endelevu juu ya njia mpya za uinjilisti, zinazowafikia watu kwa njia ya mtandao na njia zingine, huku tukitii maelekezo ya kujitenga na mikusanyiko, lakini tukidumisha mkazo wetu wenye nguvu juu ya Kristo, Neno lake, Haki yake, Huduma yake ya patakatifu, na nguvu yake ya kuokoa katika pambano kuu.

5. Tuombe ili tuweze kujua namna ya kushiriki na wengine kwa vitendo Ujumbe wa Malaika Watatu sambamba na ujumbe wa afya, kwani ujumbe huu unafaa kwa wakati huu katika historia ya dunia.

SIKU YA 10 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumapili, Aprili 05, 2020

“Mradi atanisitiri bandani mwake siku ya mabaya, Atanisitiri katika sitara ya hema yake, Na kuniinua juu ya mwamba (Zaburi 27:5)”

PP 493
Mungu atafanya mambo makubwa kwa wale wanaomtumainia. Sababu kwa nini watu wake wanaomkiri hawana nguvu kubwa ni kwamba wanatumainia zaidi hekima yao wenyewe, na hawampi Bwana fursa ya kudhihirisha uweza wake kwa niaba yao. Atawasaidia watoto wake wanaomwamini katika kila dharura ikiwa wataweka tumaini lao lote kwake na kumtii kwa uaminifu.

1. Omba kwa ajili ya washiriki wa kanisa katika nchi ya Fiji wanaotafuta kuwa nuru hata katikati ya machafuko ya ulimwengu. Omba ili kwamba wawe nguzo za tumaini na nanga za uimara katika nyakati hizi ngumu, wakiakisi upendo wa Mungu kwa wote wanaokutana nao.

2. Omba kwa ajili ya Kituo Mahalia cha Hope ili kiwe kituo cha habari kinachoaminika katika kisiwa kizima cha Fiji na kwamba Mungu atakitumia kuwafikia wengi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

3. Omba kwa ajili ya Wamisionari Wanafunzi ulimwenguni kote wanaokabiliana na janga la COVID-19 wakiwa mbali na nyumbani na wapendwa wao. Tuombee nguvu na ujasiri wa wamisionari wetu.

4. Tuombe kwa ajili ya mahitaji ya wale wanaoendelea kupoteza kazi, wanaoachishwa, na wale ambao hawajui watalipaje kodi za nyumba na bili mabalimbali, na kununua chakula wakati hawana kazi.

5. Tuwaombee washiriki wa kanisa nchini Italia, Ufaransa, Hispania, Ujerumani, na nchi zingine za Ulaya waliopoteza wapendwa wao katika janga la Coronavirus. Omba kwa ajili ya faraja na nguvu ya kuinuka na kusonga mbela.

SIKU YA 11 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumatatu, Aprili 06, 2020

“Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; 8 kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa (Mathayo 7:7, 8)”

COL 148
“Upinde wa mvua unaokizunguka kiti cha enzi ni uhakikisho kwamba Mungu ni kweli, kwamba ndani yake hakuna kubadilikabadilika, wala kivuli cha kugeuka. Tumetenda dhambi dhidi yake, na hatustahili kupokea baraka zake; na bado ni yeye aliyeweka ndani ya midomo yetu lile ombi la ajabu, ‘Usituchukie, kwa ajili ya jina lako; usikifedheheshe kiti cha enzi cha utukufu wako, kumbuka, usilivunje agano ulilofanya nasi.’ (Yeremia 14:21). Tunapokuja kwake tukiungama kutostahili kwetu na dhambi, ameahidi mwenyewe kwamba atasikia kilio chetu. Heshima ya kiti chake cha enzi imefunfamanishwa na utimilifu wa neno lake kwetu.”

1. Omba kwa ajili ya janga la afya lilaloendelea kote katika Amerika na Ulaya. Omba ili kwamba wataalamu wa afya waweze kupata mahitaji ya kutosha kama yanavyohitajika.

2. Omba kwa ajili ya wataalamu wa afya, wana usalama na watumishi muhimu wa serikali katika Amerika na duniani kote ambao wameambukizwa COVID-19 wakiwa kwenye majukumu ya kuwahudumia wengine. Tuwaombee wapone.

3. Tuwaombee wale wanaoishi peke yao wakati wa hili janga la afya, wanaopambana na hofu, na wale wanaoumia kwa kutengwa. Omba kwamba waweze kugundua kuwa hawako pekee yao, bali Yesu yuko pembeni yao.

4. Omba kwa ajili ya makanisa yote katika eneo lako mahalia ambayo inawezekana yamefungwa kwa sababu ya virusi. Tuombe ili makusanyiko yaweze kutafuta njia za kuwa “pamoja” kwa njia ya mtandao wakiwa mubashara na kushuhudia wakizingatia umbali unaofaa “social distancing” ili watu wengi zaidi waweze kuvutwa kwenye ukweli wakati wa janga hili.

5. Tuombe kwamba Mungu awashe moto mpya wa upendo ndani ya mioyo ya watu wake – upendo mpya kwa Neno lake, kwa maombi na kwa ajili ya utume.

SIKU YA 12 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumanne, Aprili 07, 2020

“Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao (2 Nyak.7:14)”

RH, Januari 03, 1907

“Washiriki wa kanisa letu wanatakiwa waongoke, ili wawe na nia ya kiroho. Mnyororo wa waumini wanaoomba kwa bidii unatakiwa uuzunguke ulimwengu. Hebu wote tuombe kwa unyenyekevu. Majirani wachache wanaweza kukutana ili kuomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Hebu wale ambao hawawezi kuondoka nyumbani, wawakusanye watoto wao, na waungane katika kujifunza kuomba pamoja. Wanaweza kudai ahadi ya mwokozi: ‘walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.’”

1. Tuombe ili kama kanisa tuweze kujua maana ya kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu na mbele zetu wenyewe. Tuombe ili atufundishe kuomba, namna ya kutubu, na kwamba uponyaji utakuja tunapomtafuta Mungu kwa mioyo yetu..

2. Tuombe kwamba Mungu atusaidie kama watu kujua maana ya kuwa na akili ya kiroho, na jinsi ya kuunda mnyororo wa maombi kuizunguka dunia.

3. Tuwaombee washiriki wanaoishi katika Konferensi ya Kusini mwa Uingereza, jijini London. Tuombe kwamba, pamoja na janga hili kufunga makanisa kuwe na ukuaji wa kanisa, kuongezeka katika kujitoa kwa Mungu na huduma, pamoja na kuwahi na kuhudhuria kila mara.

4. Tuwaombee vijana wetu wa Ulaya yote, ili warudi kanisani na wazazi wawe kielelezo imara na chanya kwa kuwaleta watoto kanisani.

5. Omba kwamba kila mtu, bila kujali umri, jinsia, mamlaka yao rasmi au hadhi, watambue kwamba inawapasa kuwa mashahidi na wajumbe wa upendo wa Mungu.

SIKU YA 13 - MAMBO YA KUOMBEA

Jumatano, Aprili 08, 2020

"Ee Mungu wetu, je! Hutawahukumu? Maana sisi hatuna uwezo juu ya jamii kubwa hii, wanaotujia juu yetu; wala hatujui tufanyeje; lakini macho yetu yatazama kwako." (2 Nyak. 20:12)

"Mungu hataki sisi tudumu tukiwa tumegandamizwa kwa huzuni ya kijinga, tukiwa na mioyo yenye vidonda na iliyovunjika. Anatutaka tutazame juu na kuuangalia uso wake mzuri wa upendo. Mwokozi mbarikiwa husimama kando ya watu wengi ambao macho yao yamepofushwa na machozi hata hawamtambui. Anatamani kutushika mikono yetu, atufanye tumwangalie kwa imani rahisi, tukimruhusu atuongoze. Moyo wake unaona huzuni zetu, uchungu wetu, na majaribu yetu. Ametupenda kwa upendo wa milele na kwa wema wenye upendo ametuzunguka kote...Tafakari juu ya hili, watoto mnaoteseka na wenye huzuni, mfurahie kwa tumaini. 'Huu ndio ushindi uushindao ulimwengu, yaani imani yetu' 1 Yohana 5:4" ***(Thoughts from the Mountain of Blessings, uk. 12)***

1. Omba kwa ajili ya waliovunjika mioyo, kwa wale waliowapoteza wapendwa wao hivi karibuni, na kwa wale wanaoshindwa kuhisi kwamba Mungu bado huko karibu.
2. Omba kwa ajili ya washiriki wa kanisa ambao wanakabili changamoto za janga la COVID-19 katika nchi nzima ya Kanada. Tuombee wapate nguvu na amani, na uponyaji. Tuombee uamsho wa kiroho ili kwamba injili isomnge mbele katika nchi yote ya Kanada kama matokeo ya hizi nyakati za changamoto.
3. Tuombe upendo usio na ubinafsi na moyo wa kutoa ili yawe ndio maisha ya washiriki wa kanisa duniani kote. Tuombe kwamba wale wenye rasilimali nyingi waweze kuwafikia na kuwapatia wale wenye chache.
4. Omba kwamba washiriki wa kanisa duniani kote waondoe tofauti zao na wakaribiane katika ushirika wa Kikristo, wakiomba kwa ajili ya Mvua ya Masika.
5. Omba kwamba washiriki wa kanisa duniani kote wabebe wajibu binafsi wa kupeleka injili kwa watu wanaowazunguka katika wakati huu ambapo mikutano ya injili imeahirishwa.

SIKU YA 14 - MAMBO YA KUOMBEA

Alhamisi, Aprili 09, 2020

“Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu (Warumi 8:18)”

AA 576
“Kupitia majaribio na mateso utukufu, tabia ya Mungu inadhihirika ndani ya wateule wake. Wanaomwamini Kristo, wanapochukiwa na kuteswa na ulimwengu, wanaelimishwa na kunidhamishwa katika shule ya K xcdcdristo. Duniani wanatembea kwenye njia nyembemba; wanatakaswa katika tanuru la mateso. Wanamfuata Kristo kwenye mapambano makali; wanastahimili kujikana nafsi na kupitia uchungu wa kuvunjika matumaini; lakini kwa njia hiyo wanajifunza hatia na ole wa dhambi, na wanaitazama kwa chuki. Kwa kuwa ni washirika wa mateso ya Kristo, wanaweza kutazama mbali kupita giza hadi kwenye utukufu wakisema, ‘Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu’ Warumi 8:18.”

1. Omba kwa ajili ya njozi ya kimbingu ili tuweze kuona mbali kupita kaburi, mbali kupita maumivu na mateso na magumu ya maisha haya, ili kuona thawabu ya mbunguni inayowangoja wale ni waaminifu hadi mwisho

   .
2. Ombea hekima kwa ajili ya wachungaji na watawala wanapotafuta kufariji watu na kuwatia moyo na kuongoza katikati ya machafuko.

3. Tuwaombee watoto wetu walio nje ya shule, na hasa wale waliotegemea vyakula walivyopata shuleni. Tuombe kwamba Mungu awainue Wakristo wanaojali ili watafute njia za kuwalisha wakati huu wa zahama.

4. Omba kwamba upendo wa Mungu ujae sana ndani yetu, utuguse sana, uvunje upya mioyo yetu, ili tusiweze kunyamaza, bali tuweze kushiriki huo upendo pamoja na wale wasio na matumaini.

5. Omba kwamba tuweze kuelewa na kuwashirikisha wengine kwa vitendo ujumbe wa “Haki kwa Imani” na kwamba tuweze kutulia katika haki ya Yesu.